

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



**WARAKA WA SPIKA KUHUSU NJIA NA UTARATIBU WA
KUENDESHA MKUTANO WA 19 WA BUNGE**

30 MACHI, 2020

WARAKA WA SPIKA KUHUSU NJIA NA UTARATIBU WA KUENDESHA MKUTANO WA 19 WA BUNGE

1.0 UTANGULIZI

Waheshimiwa Wajumbe,

1.1 Nchi yetu kwa sasa ni miongoni mwa nchi zinazopambana na ugonjwa wa Corona. Kwa wakati huo huo Bunge lina jukumu la kupitisha Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, kutunga Sheria kwa kupitisha Miswada ya Sheria pamoja na Hoja mbalimbali. Aidha, Waheshimiwa Wabunge wana jukumu la kuwawakilisha Wananchi Bungeni kwa kutoa maoni, ushauri na kuwasilisha masuala mengine yenye maslahi kwa Wananchi wanaowawakilisha na Taifa kwa ujumla.

Hivyo, pamoja na jitihada zinazoendelea za kukabiliana na ugonjwa wa Corona, Bunge inabidi liendelee na kazi.

- 1.2** Kwa kuwa ugonjwa huo ni rahisi kuambukizwa kwenye mkusanyiko wa Watu, tutaweka pembeni matumizi ya Kanuni na taratibu mbalimalil za Bunge na hivyo utaratibu wa uendeshaji wa Mkutano wa 19 wa Bunge utakuwa tofauti na utaratibu wa kawaida wa Vikao vya Bunge.
- 1.3** Kwa mamlaka niliyonayo chini ya Kanuni ya 5 ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016 nimelazimika kuchukua hatua kuu mbili kama ifuatavyo:-

- (a) kupunguza idadi ya Wabunge watakuwa wanaingia ndani ya Ukumbi wa Bunge kwa wakati mmoja; na
- (b) kupunguza muda wa Wabunge kuwepo kwenye Ukumbi na maeneo ya Bunge ili kupunguza uwezekano wa kuwaweka kwenye hatari ya kupata maambukizi hayo.

Ufafanuzi wa utaratibu utakaotumika kwenye Mkutano wa 19 ni kama inavyoonekana katika sehemu inayofuata.

2.0 UTARATIBU WA UENDESHAJI WA MKUTANO WA 19 WA BUNGE

2.1 Idadi ya Siku za Mkutano

Mkutano wa 19 wa Bunge utaanza tarehe 31 Machi, 2020 kama ilivyopangwa, na utakamilika tarehe 30 Juni, 2020. Siku zote za Mkutano zitakuwa 92, ambapo siku za kazi ni 64 na zinazosalia ni siku za mwisho wa wiki, sikukuu na mapumziko mbalimbali ya Kitaifa.

2.2 Muda wa Vikao vya Bunge

- (a) Muda wa Waheshimiwa Wabunge kuwa ndani ya Ukumbi wa Bunge umepunguzwa kutoka takriban masaa tisa hadi masaa manne;
- (b) Nyaraka na taarifa zote zitakazowasilishwa Bungeni kwa majadiliano katika Kikao husika, zitatumwa kwa

Waheshimiwa Wabunge wote kwenye *Tablet* zao asubuhi ya siku husika. Hii ni pamoja na Randama na majibu kwa Maswali ya Waheshimiwa Wabunge yaliyopangwa kwa siku hiyo;

- (c) Vikao vya Bunge vitaanza saa 8:00 Mchana na kuahirishwa saa 12:00 Jioni; na
- (d) Muda wa asubuhi utatumwa na Waheshimiwa Wabunge kusoma nyaraka zilizotumwa kwenye *Tablet* zao na kijiandaa kwa michango.

2.3 Uingiaji Ndani ya Ukumbi wa Bunge

Kama ilivyoainishwa awali, sio Waheshimiwa Wabunge wote wataingia ndani ya Ukumbi wa Bunge kila siku, badala yake utaratibu utakuwa kama ifuatavyo:-

(a) Wabunge watakaoingia Ndani ya Ukumbi wa Bunge

Kwa kila Kikao cha Bunge, Waheshimiwa Wabunge takriban 150 tu ndio wataingia kwenye Ukumbi wa Bunge kama ifuatavyo:-

- (i) Mhe. Spika;
- (ii) Naibu Spika na Wenyejuki wa Bunge;
- (iii) Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni;
- (iv) Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni;
- (v) Mnadhimu wa Chama Tawala na Mnadhimu wa Kambi Rasmi ya Upinzani;

- (vi) Waziri wa Fedha na Mipango na Naibu Waziri wake;
- (vii) Waziri mwenye Hoja husika na Naibu/Manaibu wake;
- (viii) Mawaziri waliosalia (au Naibu Waziri);
- (ix) Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa na Vyama vyao kuchangia (kwa kusema) hoja inayojadiliwa kwenye Kikao husika;
- (x) Wajumbe watano kutoka kila Kamati ya Kudumu watakaoteuliwa na Kamati husika;
- (xi) Wajumbe wa Kamati ya Bajeti; na
- (xii) Wajumbe wa Kamati ya Kisekta inayosimamia Wizara husika.

Kwa Kikao cha Kwanza kitakachoanza saa 3:00 Asubuhi tarehe 31 Machi, 2020 Wabunge watakaoingia kwenye Ukumbi wa Bunge ni:-

- (a) Mhe. Spika;
- (b) Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni;
- (c) Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni;
- (d) Wanadhimu wa kila Chama;
- (e) Mawaziri na Naibu Mawaziri;
- (f) Mawaziri Vivuli na Manaibu wao;
- (g) Kamati ya Uongozi;
- (h) Wajumbe wa Tume ya Bunge; na
- (i) Makamu Wenye viti wa Kamati.

(b) Wabunge watakuwa Nje ya Ukumbi wa Bunge

Waheshimiwa Wabunge ambao hawataingia ndani ya Ukumbi wa Bunge, watafuatilia Shughuli za Bunge kuititia Runinga katika Kumbi na maeneo mengine yaliyopangwa. Maeneo hayo ni:-

- (i) Ukumbi wa Msekwa;
- (ii) Ukumbi wa Msekwa D;
- (iii) Ukumbi wa Msekwa C;
- (iv) Ukumbi Na. 9 na 231 (Jengo la Utawala);
- (v) Ukumbi Na. 49 na 50 (Jengo la Utawala Annex);
- (vi) Ukumbi wa Mgahawa Utawala Annex; na
- (vii) *Basement* ya Ukumbi wa Bunge.

Wabunge hawa watachangia Hoja zinazowasilishwa Bungeni kwa maandishi kuititia *Tablet* zao. Kila Ukumbi utakuwa na Katibu Kamati na Watalaam wa TEHAMA kwa ajili ya kuhudumia Waheshimiwa Wabunge kwa masuala ya kiutawala na TEHAMA.

2.4 Mahudhurio ya Wabunge

Utaratibu wa kupata mahudhurio ya Wabunge utakuwa katika njia zifuatazo:-

- (a) *Head checking* itakayofanywa na Makatibu waliopangwa kuhudumia Kumbi zitakazotumiwa na Waheshimiwa Wabunge;

- (b) Mheshimiwa Mbunge kuingia (*log in*) kwenye Mfumo wa Bunge Mtandao; na
- (c) Kwa siku ambazo Bajeti ya Wizara inapigiwa kura mahudhurio ya Wabunge yatahesabiwa pia kwa Mbunge kuingia kwenye Mfumo na kupiga kura kwa kubonyeza kitufe cha kupigia kura kwenye *Tablet* yake.

Kwa Mkutano huu wa 19 matumizi ya Mfumo wa *Biometric* yatasitishwa.

2.5 Utaratibu Kuhusu Maswali

Hakutakuwa na Maswali yatakayojibiwa kwa mdomo, badala yake utaratibu utakuwa kama ifuatavyo:-

- (a) Asubuhi ya kila siku ya Kikao Wabunge wote watatumwa kwa maandishi Orodha ya Maswali yote ya siku hiyo pamoja na Majibu ya Maswali hayo sambamba na Orodha ya Shughuli;
- (b) Mbunge mwenye Swali anaweza kuuliza Maswali ya Nyongeza yasiyozidi mawili kwa maandishi kuitia Mfumo wa Bunge Mtandao kwenye *Tablet* yake;
- (c) Muda wa kutuma Maswali ya Nyongeza ni kuanzia saa 3:00 Asubuhi hadi saa 4:30 Asubuhi ili kutoa fursa kwa Wizara kuandaa Majibu kwa Maswali hayo;

- (d) Majibu ya Maswali ya Nyongeza yatatolewa pia kwa Maandishi na yatapokelewa na Katibu wa Bunge na kutumwa kwa Wabunge wote kwenye *Tablet* zao. Muda wa mwisho kwa Wizara kutuma majibu ya Maswali ya Nyongeza ni saa 7:00 Mchana; na
- (e) Maswali ya msingi kwa siku yatakuwa 10 kama kawaida.

Kwa Mkutano wa 19 hakutakuwa na Maswali kwa Waziri Mkuu.

2.6 Utaratibu kuhusu Hoja Mbalimbali

Shughuli za Bajeti za Wizara, Bajeti ya Serikali, Miswada ya Sheria na shughuli nyingine zitaanza saa 8:00 Mchana hadi saa 12:00 Jioni kwa utaratibu ufuatao:-

- (a) Asubuhi ya siku ambayo hoja husika inawasilishwa Bungeni, Wabunge watatumwa nakala ya Randama pamoja viambatisho vyote vinavyohusiana na Hoja hiyo;
- (b) Hotuba ya Waziri, Taarifa ya Kamati pamoja na Maoni ya Kambi ya Upinzani kwa Wizara husika zitatumwa kwa Wabunge wote mara tu baada ya kuanza kusomwa Bungeni yaani kuanzia saa 8:00 Mchana;
- (c) Michango ya maandishi kwa Hoja ya Kikao husika itaanza kupokelewa kuanzia asubuhi baada ya

Randama na Nyaraka nyingine kutumwa kwa Waheshimiwa Wabunge;

- (d) Mtoa Hoja atakapoanza kuhitimisha Hoja yake ndio itakuwa mwisho wa michango ya maandishi kupokelewa;
- (e) Mtoa hoja atawasilisha hoja yake kwa muda usiozidi dakika 30 isipokuwa Spika anaweza kuelekeza vinginevyo kulingana na mazingira ya Hoja husika;
- (f) Mwenyekiti wa Kamati na Msemaji wa Kambi ya Upinzani watawasilisha maoni yao kwa muda usiozidi dakika 20 kila mmoja;
- (g) Uchangiaji wa jumla utakuwa dakika 110 ambapo kila Mbunge atachangia kwa muda usiozidi dakika 10. Inakadiriwa kuwa wachangiaji 11 watapata nafasi ya kuchangia kwa siku zenye mawasilisho na upigaji kura na takriban wachangiaji 20 kwa siku nyingine;
- (h) Mtoa hoja atahitimisha hoja yake kwa muda usiozidi dakika 30;
- (i) Baada ya Mtoa Hoja kuhitimisha hoja yake, Waheshimiwa Wabunge walioandalowi na Vyama vyao, kwa ajili ya kuomba ufanuzi wa suala mahsusili sera au kifungu chenye mshahara wa Waziri, watapewa nafasi kwa kuzingatia uwiano wa vyama

kwa muda usiozidi dakika 30 na ufanuzi utatolewa humo humo Bungeni (*interactive session*); na

- (j) Kwa siku zenyе Miswada ya Sheria, Waheshimiwa Wabunge wenye marekebishо katika Muswada pia watapewa nafasi ya kutoa ufanuzi kuhusu marekebishо yao kwa muda usiozidi dakika 30.

Kwa Mkutano huu wa 19 Kanuni kuhusu Kamati ya Matumizi na Kamati ya Bunge Zima hazitatumika na badala yake baada ya kukamilika kwa hatua zote zilizoainishwa, Spika atawahoji Waheshimiwa Wabunge kwa fungu lote (Bajeti) au Muswada wote.

Baada ya Shughuli za Kikao kukamilika Spika atabaki na dakika zisizopungua 10 kabla ya muda wa kuhitimisha Bunge (*Speakers Control Time*). Spika ana mamlaka ya kuruhusu sehemu ya muda huu kutumiwa na Mbunge ye yeyote kuwasilisha “Maelezo Binafsi” kwa mujibu wa Kanuni au shughuli nyingine kwa kadri atakavyoona inafaa.

2.7 Utaratibu wa Kupiga Kura

- (a) Utaratibu wa kupiga kura kwa Bajeti za Wizara utakuwa kama ifuatavyo:-
- (i) Wabunge walioko ndani ya Ukumbi wa Bunge na ambao watakuwa nje ya Ukumbi watapiga kura ya NDIYO au SIYO kwa kubonyeza kitufe cha kupigia kura kwenye *Tablet* zao. Mfumo wa Bunge

utawezesha Spika kuona idadi ya kura inavyoongezeka kwa kadri kura zinavyoendelea kupigwa;

- (ii) Mfumo umeweka njia ya udhibiti ambapo kila Mbunge atapiga kura moja tu kwa kila hoja inayopigiwa kura;
 - (iii) Matokeo ya kura yatatangazwa na Spika baada ya zoezi la kupiga kura kufungwa; na
 - (iv) Zoezi la kupiga kura litaanza kuanzia saa 8:00 Mchana siku ambayo hoja husika inajadiliwa na litakamilika baada ya Mtoa Hoja kuhitimisha hoja yake.
- (b) Utaratibu wa kupigia kura Bajeti Kuu ya Serikali utakuwa kama ifuatavyo:-
- (i) Kura zitaendelea kuwa za wazi kama inavyoainishwa kwenye Kanuni za Bunge;
 - (ii) Waheshimiwa Wabunge wataingia ndani ya ukumbi kwa mafungu kwa utaratibu utakaotangazwa;
 - (iii) Kila Mbunge atapewa fursa ya kupiga kura kwa sauti baada ya kuitwa jina; na

- (iv) Matokeo ya Kura zitakazopigwa yatatangazwa na Spika kama kawaida.
- (c) Utaratibu wa kupigia kura Miswada ya Sheria utakuwa kama ilivyo katika Aya ya (a) hapo juu kuhusiana na kupigia kura Bajeti za Wizara.

3.0 HITIMISHO

Ni matumaini yangu kuwa Waheshimiwa Wabunge, Serikali na wadau wote wanaohusika na Shughuli za Bunge tutatoa ushirikiano na kila mmoja kutekeleza yampasayo ili kufanikisha uendeshaji bora wa Mkutano wa 19 bila kuathiri afya za Waheshimiwa Wabunge na umma kwa ujumla.

Job Y. Ndugai, Mb
SPIKA

30 Machi, 2020